Je, Tuko Salama?

Wananchi watoa taarifa kuhusu hali ya usalama wa nchi

1. Utangulizi

Fungua gazeti la siku yoyote, utakuta habari inayohusiana na vurugu au wizi. Kwa mfano, vichwa vya habari kwenye Gazeti la *The Citizen* la tarehe 7 Januari, 2014 vilikuwa ni pamoja na "Polisi yawatafuta majambazi waliowaua waendesha pikipiki wawili (bodaboda)", " Wafuasi wa Chadema wanyukana Dar" na "Mtu mmoja amefariki, Polisi waingia mgodini kutuliza ghasia za makundi ya watu wanaofanya vurugu na uporaji mgodini". Hata hivyo, inasemekana magazeti hupenda kuongeza chumvi kwenye habari, na kuyaandika matukio kwa kukuza vichwa vya habari kuliko kupata usahihi na urari wa habari yenyewe. Ni mara ngapi kiuhalisia watu wamekuwa wahanga au mashuhuda wa uhalifu? Watu huchukua hatua gani wakati uhalifu unapotokea? Je, watu wanaamini kuwa wanaweza kuutegemea mfumo unaosimamia haki?

Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza Afrika kwa njia ya simu mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa, unatafuta majibu ya maswali haya na mengine kuhusu usalama Tanzania Bara. Muhtasari huu unawasilisha mambo tisa ya ukweli kuhusu usalama nchini Tanzania kwa kutumia takwimu za hivi karibuni. Matokeo haya yametoka kwenye awamu ya nane ya utafiti wa *Sauti za Wananchi* (www.twaweza.org/sauti). Simu zilipigwa kati ya tarehe 3 na 17 Oktoba 2013; takwimu hizi ni pamoja na majibu kutoka kaya 1662. Muhtasari huu pia unatoa matokeo kutoka kwenye utafiti wa "*Afrobarometer*"na utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi* uliofanyika kati ya mwezi Oktoba na Desemba 2012.

Matokeo muhimu, yaliyotokana na taarifa za wahojiwa, ni:

- Watanzania 49% hawajawahi kuibiwa chochote, lakini Watanzania 20% wameshawahi kuibiwa kitu ndani ya kipindi cha miezi sita iliyopita;
- Watanzania 46% wameshawahi kushuhudia vurugu ndani ya jamii hivi karibuni;
- Zaidi ya nusu ya vijiji (au mitaa) yote nchini Tanzania, haina afisa wa polisi aliyepangwa huko;
- Watanzania hawafahamu namba za dharura za polisi au jeshi la zimamoto;
- Rushwa na kuchelewa kushughulikia taarifa za wananchi vimetajwa kuwa ni vikwazo vikuu kwenye utoaji taarifa za uhalifu kwa polisi;
- Watanzania 45% wamewahi kuhisi kutokuwa salama angalau mara moja wanapotembea kwenye mitaa yao ndani ya mwaka uliopita;

Muhtasari huu umeandikwa na kutayarishwa na
Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania. Imetolewa Machi 2014

SLP 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
S: +255 22 266 4301
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

2. Mambo tisa kuhusu usalama nchini Tanzania

Jambo la 1: Watanzania 20% wameripoti kesi za wizi katika miezi sita iliyopita

Kwa ajili ya ukuaji wa uchumi endelevu, usalama wa mtu au fedha na mali za jamii ni muhimu sana: Usalama bora na wa uhakika hupunguza gharama za ulinzi na ni kivutio kizuri cha watu kuwekeza. Kama Kielelezo 1 kinavyoonesha, Mtanzania mmoja kati ya wawili hajawahi kuibiwa kitu chochote. Hata hivyo, Mtanzania mmoja kati ya watano amewahi kuibiwa kitu cha thamani katika miezi sita iliyopita.

Kielelezo cha 1: Ni lini mara ya mwisho uliibiwa fedha au kitu cha thamani?

Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Utafiti wa Afrobarometer (www.afrobarometer.org) unaweza kutumika kuonyesha mtazamo wa muda mrefu, angalia Kielelezo 2. Afrobarometer iliuliza kama kuna mtu yeyote katika familia ya mhojiwa aliyewahi kuibiwa kitu chochote nyumbani ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Takwimu zinaonesha kuwa, kuna ongezeka la matukio ya wizi nchini Tanzania tangu mwaka 2005. Takwimu za Afrobarometer pia zinaonesha kuwa wizi nchini Tanzania kwa sasa ni zaidi ya wastani wa matukio ya jumla ya wizi barani Afrika (36% Tanzania, kulinganisha na 26% barani Afrika).

Kielelezo cha 2: Kukumbwa na tukio la wizi nyumbani



Chanzo: Utafiti wa Afrobarometer

Jambo la 2: Watanzania wengi wameshuhudia vurugu katika jamii hivi karibuni

Karibu nusu ya Watanzania (46%) wameripoti kuwa wameshuhudia vurugu katika jamii ndani ya miezi sita iliyopita.

Kielelezo cha 3: Ni lini mara ya mwisho wewe au mmoja wa wana familia yako wameshuhudia vurugu kwenye jamii?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Ni watu wachache tu walio na uelewa wa matukio ya usalama yaliyoripotiwa nchini kupitia vyombo vya habari. Wahojiwa walitoa taarifa kuwa wanayafahamu matukio yafuatayo: Mabomu ya Arusha kanisani (Mei 2013, 17%); Maandamano ya gesi Mtwara (Juni 2013, 13%); Mabomu katika mkutano wa hadhara wa Chadema Arusha (Juni 2013, 11%) na mashambulizi ya Zanzibar ya kutumia tindikali kwa Waingereza wanaofanyakazi za kujitolea (Agosti 2013, 8%).

Jambo la 3: Zaidi ya nusu ya jamii za Tanzania hazina maafisa wa polisi

Kwa mujibu wa mahojiano na watendaji wa vijijini na wenyekiti wa vitongoji (mitaa) 62% ya jamii za Tanzania hawana afisa wa polisi aliyepangwa kutumikia maeneo yao. Hali ni mbaya zaidi maeneo ya vijijini ambako 76% ya vijiji vimeripoti kutokuwa na afisa wa polisi aliyepangwa huko.

Kielelezo cha 4: Idadi ya polisi kwenye kijiji/mtaa



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa Awali-Jamii, Oktoba-Desemba 2012.

Jambo la 4: Watanzania hawafahamu namba za simu za dharura za polisi na kikosi cha zimamoto

Matukio ya uhalifu na moto hutokea bila kutarajia, lakini pindi yatokeapo polisi na kikosi cha zimamoto mara nyingi huwa katika nafasi nzuri ya kuyadhibiti kuliko wananchi wa kawaida. Matumizi ya simu za mkononi yameongezeka zaidi, hivyo Watanzania wengi wanapaswa kuwa na njia ya kuwasiliana na polisi na huduma za zimamoto. Hata hivyo, ni 15% tu ya wananchi wanaojua namba za dharura za polisi, wakati 6% tu ndiyo wanaojua namba za dharura za kikosi cha zimamoto. Utafiti wetu haukuhoji kuhusu utendaji wa namba hizi za dharura.

Kielelezo cha 5: Unafahamu namba za simu za dharura za polisi na kikosi cha zimamoto?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Jambo la 5: Katika matukio ya uhalifu Watanzania 47% huripoti kwanza polisi

Walipoulizwa wangekimbilia wapi endapo wangekuwa wahanga wa uhalifu, Watanzania wengi walitaja polisi na taasisi za ulinzi na usalama za kijamii. Wakazi wengi wa mijini walitaja polisi kuwa ni sehemu ya kwanza ya kukimbilia. Ingawa wakazi wa vijijini pia kwa kiasi kikubwa walitaja polisi, idadi kama hiyo walisema wangeenda kuripoti katika asasi za kijamii za ulinzi na usalama. Wachache sana walionyesha hawajui wangeripoti kwa nani.

Kielelezo cha 6: Kama ungekuwa mhanga wa uhalifu hapa nchini ungekwenda wapi kwanza kuomba msaada?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Jambo la 6: Rushwa na mwitikio duni ni vikwazo vya kuripoti matukio ya uhalifu

Wahojiwa wa Sauti za Wananchi waliombwa kuonesha ni vikwazo gani, kama vilikuwepo, ambavyo walifikiri wananchi wangeweza kukutana navyo wakati wa kutoa taarifa ya uhalifu polisi.

Kielelezo cha 7: Ni sababu gani kubwa zinazowafanya watu wengi wasiripoti polisi uhalifu kama wizi au uvamizi unapotokea?

Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Waliohojiwa walitaja mambo makuu mawili yafuatayo: polisi huomba rushwa (22%) na polisi hawawasikilizi wala kuwajali (22%). Kwa upande mwingine, washiriki 16% walieleza kuwa watu wenyewe hawatoi taarifa za uhalifu polisi. Tunaona kwamba idadi hizi zinatofautiana kwa kiasi fulani na matokeo ya utafiti wa Afrobarometer wa mwaka 2012, ambapo umbali wa vituo vya polisi ulitajwa kuwa kikwazo kikubwa.

Jambo la 7: Mauaji mara nyingi huhusishwa na makundi ya watu

Walipoulizwa endapo wamewahi kusikia kuhusu mtu yeyote katika kitongoji chao katishiwa kuuawa, kapigwa, au kapigwa na mawe na ama Polisi jamii, mwananchi wa kawaida, kundi la watu, polisi au jeshi, 54% walisema ndiyo. Aidha 31% walikiri kuwa waliwahi kusikia mtu katika mtaa/kitongoji chao ameuawa na moja ya makundi hayo. Katika matukio ya mtu kuuawa, hii iliripotiwa mara nyingi (19%) kufanywa na makundi ya watu. Na katika matukio ya kutishiwa, kupigwa au kupondwa mawe, hii iliripotiwa mara nyingi hufanywa na polisi jamii (31%).

Kielezo cha 8: Nani anafanya uhalifu?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Kumbuka kuwa idadi hizi hazitokani na uchunguzi wa moja kwa moja wa kushuhudia bali ni matukio ambayo "yamekua yakisikika" kutoka kwa wahojiwa. Kwa kuzingatia ukweli huu, takwimu hizi zina maana kuwa Mtanzania kwa wastani anaweza kutishiwa, kupigwa au kuuawa na wananchi wenzake au kikundi cha raia kuliko na polisi au wanajeshi.

Wananchi pia waliulizwa uelewa wao wa mazingira ambayo matukio haya yanatokea. Tukitazama mauaji yatokanayo na kundi au mtu binafsi, taarifa za msingi zinazotolewa kueleza tukio kama hilo katika matukio mengi ni wizi (74% kundi la watu kumwadhibu mwizi, 47% mtu binafsi kumwadhibu mwizi).

Jambo la 8: Watanzania wengi hawauamini mfumo wa sheria

Je, Watanzania wanaamini kuwa mtu aliyefanya uhalifu ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria? Kielelezo cha 9 kinaonesha kuwa; kwanza, wahojiwa wana imani ndogo sana kama mtu *yeyote* ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Pili, kuna mtazamo wa kwamba watu matajiri na wenye uwezo ni rahisi zaidi wao kukwepa adhabu kuliko wananchi wa kawaida.

Kielelezo cha 9: Iwapo mtu miongoni mwa hawa wafuatao ataiba au kufanya uhalifu wowote ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Jambo la 9: Watanzania wengi wana wasiwasi kuhusu usalama wao kwenye jamii zao

Kwa ujumla, wahojiwa 39% waliripoti kuhofia uhalifu katika nyumba zao, wahojiwa 45% wakisema kuwa angalau mara moja walihisi hawako salama kutembea katika maeneo ya mitaa yao. Hii inaakisi takwimu za utafiti wa Afrobarometer ambazo zilionesha kuwa, Watanzania 43% wana hofu ya uhalifu katika nyumba zao. Takwimu za utafiti wa Afrobarometer zinaonesha zaidi kuwa, takwimu hizi kwa Tanzania ziko juu ikilinganishwa na wastani wa Afrika wa 32%

Kielelezo cha 10: Kwa kipindi cha mwaka uliopita, ni mara ngapi umewahi kuogopa au kuhisi hauko salama?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

Inaonekana kuwa wananchi wana hofu zaidi kipindi cha uchaguzi. Kwa mfano, zaidi ya nusu (57%) ya washiriki walionesha hofu ya kuwa wahanga wa ghasia za kisiasa, ikilinganishwa na 45% ambao walihisi hawako salama kutembea katika mitaa yao angalau mara moja kwa kipindi cha mwaka uliopita.

Kielelezo cha 11: Kipindi cha uchaguzi mkuu uliopita ulihofia kuwa mhanga wa ghasia za uchaguzi?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi Awamu ya 8, Oktoba 2013.

3. Hitimisho

Ripoti hii fupi juu ya usalama imetokana na hali halisi ya uzoefu na wananchi wa Tanzania Bara. Muhtasari huu umebaini kuwa kama ilivyo katika jamii nyingine nyingi Watanzania wanakabiliwa na uhalifu na hofu: fedha na vitu vingine vya thamani wakati mwingine huibwa kutoka kwa wananchi, na wanashuhudia na kusikia visa vya vurugu katika mitaa/vitongoji vyao.

Kwa kuwa Serikali ina mamlaka juu ya matumizi ya nguvu, wananchi wanatakiwa kuripoti matukio haya kwa polisi ambao wanalo jukumu la kulinda amani, kusimamia utekelezaji wa sheria, kulinda watu na mali zao pamoja na kuchunguza uhalifu. Ili haki itendeke kwa mujibu wa sheria baada ya uhalifu kufanyika, mhusika anapaswa atambulike, akamatwe na kisha atiwe hatiani na ahukumiwe na mahakama kwa mujibu wa sheria.

Wananchi wa Tanzania huwatafuta polisi ili kupata msaada lakini kuufikia mfumo rasmi wa ulinzi na usalama siyo rahisi, hasa katika maeneo ya vijijini. Katika vijiji vingi hakuna maafisa polisi. Kwa ujumla, maafisa wengi wa polisi mara zote hawaonekani kuwa ni wa msaada wowote, na watu wengi hawajui namba za simu za dharura za polisi au kikosi cha zimamoto.

Matokeo yake, watu mara nyingi wanaamua kutumia njia “zisizo rasmi” kushughulikia wale waliobainika kuwa ni wahalifu. Siyo jambo geni kwa Watanzania kusikia habari za mtu fulani katika mtaa/kitongoji chao kauawa na kundi la watu. Matukio haya mara nyingi hutokana na vitendo vya wizi. Kwa upande mwingine, ni ukweli kwamba Watanzania wengi hawaamini kuwa wahalifu wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria, hasa kama ni matajiri au watu wenye madaraka.

Kuwa na imani ndogo katika mfumo wa sheria na njia zisizo rasmi za kupata haki kutumika, nchi inakabiliwa na changamoto kubwa kuwakikishia usalama wananchi. Upanuzi wa mifumo rasmi ya usalama na kuipatia sekta rasilimali za kutosha inaweza kuwa sehemu ya ufumbuzi, ila hali inahitaji ubunifu zaidi na kufikiri kwa mapana. Hii inaweza kuwa ni pamoja na kupanua huduma ya polisi jamii - ambayo inasisitiza ushirikiano wa karibu kati ya polisi na raia; vikundi vya kijadi vya usalama vyenye kanuni nzuri za usimamizi wa sheria; na kuhimiza njia ambazo muundo mkuu wa kimamlaka wa Serikali za mitaa (kwa mfano; mabaraza ya vijiji, kamati za shule) zinaweza kutumika zaidi kusikiliza sauti na matakwa ya wananchi. Masuala haya yanahitaji mjadala mkubwa wa umma, ikiwa ni pamoja na kwenye michakato ya Bunge la Katiba.